Mwongozo Muhimu

Jukumu la kupunguza umasikini na kuyafikia Malengo ya Millennium ya Maendeleo ni kubwa sana.

Ingawa kumekuwa na mafanikio makuu katika kuupunguza umasikini katika miongo miwili iliyopita—kiasi cha umasikini kilipungua kwa watu milioni 200 katika miongo miwili iliyopita—watu bilioni 1.2 bado wanaishi kwa pato la chini ya $1 kwa siku, wakati wengine milioni 2.8 wanaishi kwa pato la chini ya $2 kwa siku. Katika miaka 50 ijayo, idadi ya watu duniani inatazamiwa kukua kutoka bilioni sita hadi tisa, na karibu na asilimia 95 ya ongezo hilo likiweko katika nchi zinazoendelea.

Malengo

Millennium Development Goals (MDG) [Malengo ya Millennium ya Maendeleo], yaliyoafikiwa na nchi 189 katika mwaka 2002 katika United Nations Millennium Summit [Mkutano wa Umoja wa Mataifa wa Millennium], kukiwa na makubaliano kuhusu yanayohitajika ili kuweza kuwa upungufu wa umasikini.Malengo yana shabaha hususa ambazo jamii yote ya maendeleo—wafadhili na wafudhiliwa, pamoja—watashughulikia.

1. Kufuta ufukara na njaa
2. Kufaulu kuwa na elimu ya msingi kwa wote
3. Kutilia nguvu usawa wa kijinsia na kuwapa wanake uwezo
4. Kupunguza vifo vya watoto
5. Kukabiliana na HIV/UKIMWI, malaria, na magonjwa mengine
6. Kuhakikisha ustawi wa mazingira
7. Kubuni ushirika wa kilimwengu wa maendelo

Haadi kufikia sasa, inaonekana kwamba lengo la kwanza—kupunguza idadi ya watu wanaoishi katika ufukara kati ya mwaka wa 1990 na 2015 na kuimarisha kupatikana kwa maji masafi—litafaulu. Hata hivyo takwimu hii inaonyesha tu kiwango cha kadiri cha ulimwengu mzima, ambapo takwimu za hakika zitakuwa tofauti ulimwenguni, na zitakuwa za chini zaidi Afrika.
Lengo la mwisho linaeleza kati ya mambo mengine majukumu ya wafadhili na wanaofadhiliwa. Mikutano zaidi ya hivi karibuni-pamoja na miwili ya 2002: International Conference on Financing for Development [Mkutano wa Kimataifa wa Ufadhili wa Maendeleo] huko Monterrey na World Summit on Sustainable Development [Mkutano wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kudumu] wa Johannesburg—imeshuhudia kutokea kwa desturi mpya, ambapo nchi zilizoendelea zimegundua umuhimu wa kupunguza vikwazo vya biashara, kuongeza usaidizi na kupunguza mzigo wa madeni. Kufikia malengo ya MDG pia kutahitaji nchi nyingi zinazoendelea ziwe na mwelekeo thabiti wa kuanzisha mifumo bora ya kiuchumi, usimamizi bora wa utumishi wa umma usio kuwa na ufisadi, na kuweko kwa hali inayovutia uwekezaji wa kibinafsi.
Jukumu la Benki ya Dunia ni ipi?
Benki ya Dunia husaidia nchi zinazoendelea na zile zilizoendelea kwa mikopo, mihakikisho, shughuli za utafiti na ushairi, usaidizi wa madeni, kukuza uwezo, pamoja na ukaguzi wa kimataifa na uteteajji.

> **Mpango wa Benki ya Dunia wa kupunguza umasikini una nia ya kubuni hali ya uwekezaji na uwekezaji kwa watu masikini.**

Strategic Framework Paper [Mkakati wa Mbinu za Mpangilio] ya mwaka 2001 ilitambua nguzo mbili ambazo Benki itastawisha shughuli za zake za mikopo, usaidizi, na kukuza uwezo ili kuweza kufikia MDG: kustawisha hali ya uwekezaji, kazi, na kukua kwa kudumu kwa uchumi, kuwekeza kwa watu masikini na kuwapa uwezo wa kushiriki katika shughuli za maendelo.
Nguzo ya kwanza imebuniwa kwa thibitisho kwamba maendeleo yakufanikiwa zaidi ni yale yaliyo ongozwa na sekta ya kibinafsi lakini yanayo kuwa ongozwa na serikali ambayo hustawisha hali murwa ya shughuli za kibiashara na mambo ya kiuchumi na hupeana miundombinu, rasilimalia za kibinadamu, na mfumo wa kisheria unaofaa.
Nguzo ya pili inaonyesha umuhimu wa afya na elimu pamoja na umuhimu wa kupunguza majanga, ikiwa masikini watashirikishwa na pia watasaidia kustawisha nafasi za kiuchumi.

Sehemu saba muhimu. Mwanzoni mwa mwaka wa 2003, usimamizi wa Benki ulieleza sehemu saba zakutilia mkazo zaidi: Elimu kwa Wote, HIV/UKIMWI, afya ya wanawake waja wazito na ya watoto, maji na usafi, hali murwa ya uwekezaji na shughuli za fedha, biashara, na uhifadhi wa mazingira.
Sehemu hizi—zilitambuliwa kuwa za umuhimu mkubwa sana katika sehemu zote zinazopokea udhamini wa Benki—ni ambazo Benki ina nia ya kuimarisha matokeo hivi karibuni. Haya ni kwa njia ya kuongeza mipango ya kukuza uwezo na kurahisisha mbinu, pamoja na namna za asili za shughuli za fedha na ufadhili wa karadha.
Wakati International Bank for Reconstruction and Development [Benki ya Marekibisho na Maendeleo] ilipobuniwa katika mwaka wa 1944, "maendeleo" yalikuwa jambo lilotokea baadaye. Kwa wakati huo, shughuli ya muhimu zaidi ya Benki ya Dunia ilikuwa ni urekebishaji wa Ulaya ya baada ya vita (vya dunia).
Ni baada ya Vita vya Pili vya Dunia ndipo desturi ya kuwa nchi tajiri zitazisaidia nchi masikini ilipoanza. Kwa miongo kadhaa tangu wakati huo, ufahamu wa jamii ya kimataifa wa uhusiano kati ya upunguzaji wa umasikini na kukua kwa uchumi umepiga hatua na kwa sasa unajumuisha ushirikiano wa kibinafsi na wa kijamii, kushiriki, kupeana uwezo na usimamizi wa kiserikali.

- **Hakuna shaka kwamba kukua kwa uchumi peke yake hakumaanishi upungufu wa umasikini.**

Katika mwaka wa 2000, Benki ya Dunia ilichapisha matokeo ya utafiti wa maana sana kuhusu umasikini. Voices of the Poor [Sauti za Masikini] ilitaka kudokeza sababu na athari za umasikiini ulimwenguni kwa kuwafikia masikini wenyewe: waume na wanawake 60,000 katika nchi 60 walipeana habari za visa vyao vya ukweli wa kuishi katika hali ya umasikini na wakaelza pia kile ambacho masikini wanayo hitaji ili kuboresha maisha yao.
Utafiti huu ulionyesha kiwango ambacho umasikini una uhusiano wa karibu sana na mambo mengine ya maendeleo ya binadamu—kwa mfano: afya, elimu, kushiriki katika serikali—na kiwango ambacho ufisadi na usimamizi mbaya wa mambo ya umma unavyokuwa na madhara.
Utafiti wa *Sauti* ulifanywa ili kuunga mkono 2000/2001 World Development Report [Ripoti ya 2000/2001 ya Ulimwengu ya Maendeleo] ya "Kuupiga Vita Umasikini" na imekuwa na mvuto katika mengi kati ya mabidiliko ya wakati huu, kama vile Benki inavyo endesha shughui zake. Ajenda mpya ya kuuupiga vita umasikini imeelezwa katika ripoti:

- Kuongeza uwezo, ambayo inamaanisha kuunga mkono ukuzaji bora wa uchumi, kufikia masoko, na kupeana huduma za jamii kwa watu masikini.
- Kupeana uwezo, ambayo inamaanisha kujumuisha na kushirikisha watu masikini, na haki na ukweli wa serikali.
- Usalama, ambao unahusu upunguzaji wa atharii zinazo wakabili watu masikini—iwe ni janga la kiuchumi, ugonjwa, mkasa wa hali ya anga, ama vita.

Maendeleo yenye Kuendeshwa na Jamii. Kati ya matokeo muhimu zaidi ya utafiti na kwamba umasikini ni hali zaidi ya kutokuwa na pato. Umasikini unamaanisha kutokuwa na 'sauti' ya kuweza kufanya uamuzi kuhusu mambo muhimu yanayo husu maisha ya masikini, ama kuto kuwa na kuwakilishwa katika vyombo vya kisiasa vya mikoa ama kitaifa.
Hii imesababisha kuongezeka kwa mweleko katika miradi ya "community-driven development" [maendeleo yenye kuendeshwa na jamii]: ambayo hupeana nafasi kwa makundi ya kijamii ya kuweza kujiongoza na kuwa na uamuzi mkubwa zaidi katika ugawaji wa fedha za kitaifa pamoja na rasilimali zake—na kwa namna hii kuepusha ufisadi—na "sauti" yenye uwezo zaidi katika taasisi. Baadhi ya mifano ni:

- Kufadhili kamati za elimu za jamii katika sehemu za mshambani El Salvador, Guatemala na Honduras, ambako wazazi wenyewe wanasimamia fedha za shule, wanahaikisha watoto wanakwenda shule, kuajiri walimu na pia kukagua matokeo ya kazi zao.
- Mpango wa kufanya usafi kitika mtaa wa mabanda katika miji mikubwa minne ya Amerika ya Kusini—Guatemala City, Caracas, Sao Paulo, na Recife—ambako makundi ya mitaani, mashiirika ya watumishi wa umma, na serikali za mikoa, pamoja na biashara za kibinafsi zinasaidia kuboresha huduma za makazi na za kijamii ili kuwe na afaya njema na kupunguza uhalifu.

Kukua [kwa uchumi] na kuongezeka kwa uwekezaji wa kijamii na wa kibinafsi, pamoja na uwekezaji katika miundombinu, kumebakia muhimu kwa kupunguza umasikini. Kwa kawaida, kufikia kwa miundombinu ya

kisasa na huduma zilizo imarishwa huimarisha matokeo katika nyanja za afya na elimu, kupunguza idadi ya vifo vya watoto kutokana na magonjwa ya kwenye maji yasiyo safi, na magonjwa ya kupumua, na kuhakisha uwezo wa kwenda shule na hazanati.

Kupiga hatua kunategemea juhudi za pamoja katika sekta mbalimbali:

- Peru, ongezeko la pato la jamii zenye uwezo wa kufikia miundombinu ni asilimia 45 zaidi kushinda lile la jamii amabzo hazipati huduma aina hiyo.
- Katika miji ya Nicaragua, katika jamii ambako iliimarishwa, vifo vya watoto vilipunga kwa asilimia 50.
- Morocco, kwenda shule kwa watoto wa kike iliongezeka zaidi ya mara mbili katika sehemu zenye barabara zenye lami.

Kwa sababu ya mahitaji makubwa na kiasi kichache cha rasilimali za Benki, jukumu sasa ni la kupanua kila chanzo cha udhamini. Kwa kushughulikia mageuzi ya sera, na shughuli za uwekezaji zilizochaguliwa, uwezekano wa kupata chanzo cha aina nyengine cha ufadhili huwa unazidi.

Comprehensive Development Framework (CDF) [**Mpango wa Pamoja wa Maendeleo**]

Kuchagua aina ya mipango katika nchi tofauti kwa sana hutegemea vipaumbele vya nchi zenyewe. Wazo la mpango wa pamoja wa maendeleo, ialiyofafanuliwa na Benki na linaloendelea kufwatwa na jumuiya yote ya maendeleo, ni msingi wa mipango yote.

Lengo muhimu la CDF ni umilikaji wa miradi wa nchi, mwelekeo na mpango kamili tena wa mda mrefu, ushirikiano wa muhimu kati ya wanahisa, na mwelekeo wa uhakika kwa matokeo ya maendeleo.

Iwe ni namna za uwekezaji kwa watu masikini na kuwapa uwezo wa kushiriki katika maendeleo ama jinsi ya kuleta hali ya uwekezaji, kazi, na kukua kwa kudumu, mafanikio makubwa zaidi yanawezekana ikiwa jukumu la matumizi kamili ya usaidizi wa kigeni liko mikononi mwa nchi zinazo pata usaidizi. Leo, wanaopata mikopo na siyo Benki, ndio wanaopanga ajenda za maendeleo wakati Benki ina jukumu la ushauri.

CDF huongoza mfumo wa maendeleo kwa kila nchi kwa kushughulikia aina zote za maendeleo—ya kijamii, kimajengo, kibinadamu, kiserikali,na kimazingira, pamoja na yale ya kiuchumi na ya kifedha. Mifumo lazima uwe na imani ya wahusika wote—watumisji wa umma na sekta ya kibinafsi, pamoja na serikali na wafadhili.

Kwa Benki, CDF huwezesha kuweko kwa miradi iliyochaguliwa kuwa na matokeo ya manufaa zaidi, na ina peana nafasi kwa Country Assistance Strategies [Mipango ya Usaidizi wa Nchi]. Binu hii—kwa kawaida ya miaka mitatu—hufafanua mipango ya Benki ya kupeana mikopo na ile isiyokuwa ya kupeana mikopo. Kwa nchi masikini, CAS na usaidizi wote—pamoja na kupunguza madeni—kwa sasa unategemea utayarishaji wa nchi zinaopokea mikopo ripoti za Poverty Reduction Strategy Papers [Mkakati wa Mbinu za Upunguzaji Umasikini], ambayo lazima iwe ya kudumu, ilenge umasikini, na iwe ni ya ushirikiano.

Mbinu za Sekta

Mwongozo wa usaidizi hauhusu nchi hadi nyengine tu, bali unapatikana sekta moja hadi nyengine. Mbinu za sekta husaidia kuunda mwelekeo wa Benkina shughuli zake katika sekta ama sehemu muhimu, kwa kutambua sehemu dhaifu za matokeo ya nchi ili ziweze kuimarishwa. Zinakamilishwa—na kugaguliwa kila miaka mitatu—baada ya majadiliano marefu, na pia yaliyo na ushiriki wa katika Mtandao.

Mbinu ya sekta ya Usafiri wa Mijini kwa sasa inafanyiwa ukaguzi.

Hivi karibuni Benki ilitoa mbinu mpya za sekta kwa Misitu, Rasilimali za Maji, Maendeleo ya Mashambani, Mazingira, Maswala ya Kijinsia, Ufundi wa Mawasiliano and Maendeleo ya Sekta ya Kibinafsi.

Mbinu zaidi za Sekta zinapatikana kwa:

Kuzuia Ufisadi
Elimu
Usimamizi na Mageuzi ya Sekta ya Umma
Afya, Lisho Bora na Ongezeko la Watu (angalia pia Mbinu ya HIV/UKIMWI ya Afrika)
Uchimbaji wa Madini (Mbinu za Nchi)
Serikali za Mjini na za Mikoa
Usimamizi wa Raasilimali za Maji